

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 22 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre, Dar es Salaam saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 3, 2022. Agenda itakuwa kama ifuatavyo:

- 22.1 MATANGAZO NA AKIDI
- 22.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
- 22.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 21 ULIOFANYIKA TAREHE 4 JUNI 2021
- 22.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 21 WA WANAHISA
- 22.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022
- 22.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2021
- 22.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI
- 22.8 KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI
- 22.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DISEMBA 2022
- 22.10 MENGINEYO

## MAELEZO MUHIMU

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima aje na nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.
2. Mjumbe anayehuswa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni kabla ya saa 4 asubuhi Alhamisi ya tarehe 2 Juni 2022.
3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atatakiwa kuhudhuria kwa gharama zake mwenyewe. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi zitapatikana matawini.
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 193 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 96.7 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2021.

## Tarehe za kuzingatia:

- Tarehe ya tangazo:** - 13 Mei 2022
- Hisa kuuzwa pamoja na gawio :** - 13 Mei 2022
- Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :** - 1 Juni 2022
- Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** - 2 Juni 2022
- Daftari la wanahisa kufungwa:** - 6 Juni 2022
- Malipo ya gawio kwa wanahisa: kuanzia tarehe** - 15 Juni 2022



Lilian R. Komwihangiro  
Katibu wa Kampuni

13 Mei 2022